**Jina la Mtahiniwa**______________________________ **Nambari**____________/__________

**7015/2** **Sahihi ya Mtahiniwa** ____________
**LUGHA YA KISWAHILI**
**Disemba 2012** **Tarehe** ________________
**Muda: Saa 1 $\frac{1}{2}$**

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

# CERTIFICATE IN EARLY CHILDHOOD DEVELOPMENT AND EDUCATION

LUGHA YA KISWAHILI

**Muda: Saa 1 $\frac{1}{2}$**

## MAAGIZO

*Andika namba na jina lako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Tia sahihi yako na tarehe kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Mtihani huu una sehemu tatu:* ***Insha, Ufahamu na Matumizi ya Lugha.***
*Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.*

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| SEHEMU | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| I | 15 | |
| II | 15 | |
| III | 20 | |
| JUMLA | 50 | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.**

*© 2012 The Kenya National Examinations Council* **Fungua ukurasa**

Powered by: www.manyamfranchise.com

## SEHEMU YA KWANZA : INSHA

(alama 15)

Jibu swali la 1 au la 2

Andika insha **moja** isiyopungua maneno **300** kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:

1. Andika hotuba utakayowatolea raia wa kata yako kuhusu suala la usalama.
2. Andika insha juu ya methali: Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.



Powered by: www.manyamfranchise.com

**SEHEMU YA PILI: UFAHAMU** (alama 15)

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Baada ya nchi yetu kupata uhuru, viongozi walijifunga kibwebwe kukabiliana na maadui watatu: ujinga, magonjwa na umaskini. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba, licha ya juhudi za viongozi na raia, maadui hawa bado wanaendelea kuitafuna jamii yetu.

Athari za maadui hawa zinahisika zaidi katika sehemu za mashambani na viunga vya miji. Sehemu za mashambani ndizo ambazo zinaendeleza kilimo. Tunaweza kudai kwamba sehemu hizi ndizo zinazopaswa kulilisha taifa. Hata hivyo, kilimo kinachoendelezwa huku kimekumbwa **na tufani kali.** Wakulima wengi wamejipata wakila hasara mwaka baada ya mwingine; kisa na maana; mvua haikunyesha, kiangazi kimekithiri na kuharibu mimea. Mathalan, miaka miwili iliyopita ilishuhudia kiangazi kikali ambacho kilisababisha vifo vya watu na wanyama.

Pamoja na kutotabirika kwa hali ya anga, wakulima wamejipata wakipigana na ushindani mkubwa kutoka kwa wafanyabiashara ambao wanaagiza vyakula kama vile mahindi na sukari na kuviuza kwa bei ya chini. Baadhi ya wakulima hulazimika kupunguza bei za vyakula vyao. Wengine hupata hasara maradufu mazao yao yanapoozea maghalani kwa kukosa masoko.

Katika baadhi ya maeneo ya mashambani, miundomsingi haijaimarika na huduma za afya zingali chini ya matarajio. Zipo sehemu ambazo zina zahanati moja tu ambayo inatoa huduma kwa vijiji kadha. Maeneo mengine, japo yana hospitali za wilaya na mikoa, hukumbwa na tatizo la msongamano wa wagonjwa. Hospitali nyingine pia hukosa vifaa vya kudhibiti magonjwa sugu, hali ambayo hulazimu wagonjwa wengine kushauriwa kutafuta matibabu katika hospitali ya kitaifa, ambako pia kumejaa wagonjwa wanaohitaji matibabu maalum. Si ajabu kupata baadhi ya wawele wakikaa hospitali kwa mwezi mzima, wakingojea huduma kama vile upasuaji.

Barabara nyingine za mashambani, ama hazipitiki kwa sababu ya mashimo, au hazijatiwa lami. Hali hii imetinga shughuli za kusafirisha watu na bidhaa. Harakati za uzalishaji mali nazo zimekwamizwa kiasi kwamba sehemu nyingi za mashambani zimebakia nyuma kimaendeleo zikilinganishwa na sehemu za mijini. Wakazi wengi wa sehemu za mashambani wamejipata wakididimia katika umaskini kila uchao.

Ingawa nchi yetu inaendelea kupiga hatua katika maendeleo ya kiviwanda, sehemu za mashambani bado ziko nyuma katika uwanja huu. Vipo viwanda vichache mno katika sehemu za mashambani ikilinganishwa na mijini ambamo mna viwanda vingi. Viwanda ni chanzo cha ajira. Vijana wengi katika sehemu za mashambani wanapokosa ajira humu, wao huhamia mijini **kuzumbua riziki**.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Wapo wale ambao hudiriki kupata ajira, ilhali wengine huambulia patupu. Baadhi katika kundi hili huamua kushiriki katika visa vya uhalifu ili kujikimu. Matokeo ni kwamba ukosefu wa usalama umekuwa jambo la kawaida kama sheria.

Hali kadhalika, wapo wakazi wa sehemu za mashambani, ambao japo wana fursa ya kujiendeleza, wana mtazamo hasi kuhusu kilimo. Kuna wale wanaodhani kuwa kilimo hakina natija, kinastahili kuachiwa wazee. Katika kumbo hili, kuna baadhi ya vijana ambao, japo wazazi wao huenda wakawa na mashamba makubwa, wao huhiari kwenda mijini kutafuta kazi afisini. Aidha, kuna wale ambao wanashiriki kilimo lakini wanakosa mbolea na pembejeo muhimu. Hali ikiwa hivi, mashamba hukosa kutoa mazao ya kutosha kulilisha taifa, janga la njaa nalo hushamiri. Si ajabu kwamba katika miaka ya hivi karibuni raia wengi wamekuwa wakitegemea misaada ya chakula kutoka ndani na nje.

Ni dhahiri kwamba sehemu za mashambani zimekumbwa na adha nyingi. Baadhi ya matatizo huenda yakawa ya kimaumbile. Hata hivyo, yapo matatizo ambayo wenyeji tu ndio wanaoweza kuyatatua. Vijana hawana budi kuhimizwa kuyawajibikia maisha yao. Badala ya kungojea serikali kuanzisha viwanda, wao wanaweza kushiriki katika miradi ya kuzistawisha sehemu hizi. Kwa mfano, wanaweza kuungana kuziba mashimo barabarani. Wanaweza pia kuwaiga vijana wenzao mjini kwa kujiajiri katika viwanda vya juakali. Wengine wanaweza pia kuanzisha kilimo cha mboga, maua au matunda ambayo yanaweza kunyunyiziwa maji badala ya kungoja hadi msimu wa mvua. Juhudi hizi zinaweza kusaidia kupunguza makali ya njaa pamoja na kuzikuza zaidi sehemu za mashambani.



Powered by: www.manyamfranchise.com

Maswali

(a) Huku ukirejelea makala, taja matatizo **sita** yanayoikumba sekta ya kilimo. (alama 6)

(b) Kwa mujibu wa kifungu, eleza faida **tatu** zinazotokana na kuimarisha sehemu za mashambani. (alama 3)

(c) Eleza masuala **manne** ambayo mwandishi ameibusha katika aya ya mwisho. (alama 4)



Powered by: www.manyamfranchise.com

(d) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu:- (alama 2)

(i) tufani kali

(ii) kuzumbua riziki.

**SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA** (alama 20)

(a) Andika katika umoja.

Magugu yale ndiyo yaliyoyavamia maziwa hayo. (alama 2)

______________________________

(b) Andika aina za maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

<u>Mimi</u> nitamsaidia <u>ingawa</u> hana shukrani kamwe.

______________________________

(c) Tunga sentensi **mbili** tofauti kuonyesha matumizi mawili ya alama ya kuulizia. (alama 2)

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

(d) Geuza sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu.
Musau aliwashauri wanafunzi wake vyema. (alama 1)

______________________________

______________________________

(e) Tunga sentensi moja kubainisha kivumishi cha sifa. (alama 1)

______________________________



Powered by: www.manyamfranchise.com

(f) Eleza maana mbili za neno: Zima (alama 2)

(g) Andika katika ukubwa. (alama 1)

Kuta za nyumba hizo zilizunguka kijiji.

(h) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi mawili tofauti ya 'na'. (alama 2)

(i) Wingu ni kwa nzige ______________ ni kwa milima. (alama 1)

(j) Andika kisawe cha neno: tweta (alama 1)

(k) Eleza maana ya methali "Ulingo wa Kwae haulindi Manda." (alama 2)

(l) Kengele zinazovaliwa miguuni na wachezaji ngoma huitwa ________________.

(alama 1)

(m) Tunaitaje?

(i) Pesa anazopewa mtu kwa kufikwa na hasara ________________.

(ii) Mtu anayetumwa kupeleka posa ________________.

(alama 2)



Powered by: www.manyamfranchise.com